# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

# BUNGE LA TANZANIA

## ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

## MKUTANO WA KUMI NA TATU

## KIKAO CHA NANE

**08 NOVEMBA, 2023**

# ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

______________________

## MKUTANO WA KUMI NA TATU

## KIKAO CHA NANE – TAREHE 08 NOVEMBA, 2023

**I. DUA:**

**II. MASWALI:**

**OFISI YA WAZIRI MKUU:**

**107. MHESHIMIWA MRISHO MASHAKA GAMBO (ARUSHA MJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kufanya mapitio ya Malipo ya Mkupuo (Kikokotoo) ya Asilimia 33 kwa Wafanyakazi.

**OFISI YA RAIS (TAMISEMI):**

**108. MHESHIMIWA AYSHAROSE NDOGHOLI MATTEMBE (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, Serikali ina mpango gani wa kukarabati Hospitali ya Wilaya ya Manyoni.

**109. MHESHIMIWA KABULA ENOCK SHITOBELA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, lini Serikali itajenga chumba maalum *Incubator* kwa ajili ya Mama na Watoto Njiti katika Hospitali ya Wilaya Ukerewe.

**110. MHESHIMIWA NICHOLAUS GEORGE NGASSA (IGUNGA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, lini Serikali itapandisha hadhi Shule ya Sekondari ya Igurubi – Igunga kuwa ya Kidato cha Tano na cha Sita.

**111. MHESHIMIWA TIMOTHEO PAUL MNZAVA (KOROGWE VIJIJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, lini Serikali itajenga Barabara ya Msambiazi – Lewa – Lusindi hadi kwa Blue kwa kiwango cha lami.

**OFISI YA RAIS (UTUMISHI NA UTAWALA BORA):**

**112. MHESHIMIWA ANNE KILANGO MALECELA (SAME MASHARIKI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (Utumishi na Utawala Bora):-

Je, kuna mkakati gani wa kutoa motisha kwa Watumishi wanaofanya kazi kwenye mazingira magumu.

**OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO NA MAZINGIRA):**

**113. MHESHIMIWA MOHAMED SAID ISSA (KONDE):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira):-

Je, kero 11 za Muungano zilizopatiwa ufumbuzi zimeleta manufaa kiasi gani katika utekelezaji kwa pande zote mbili.

**WIZARA YA KILIMO:**

**114. MHESHIMIWA YAHAYA OMARY MASSARE (MANYONI MAGHARIBI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo:-

Je, lini Tume ya Umwagiliaji itatimiza ahadi yake ya kuvuna maji ya mvua katika Mbuga inayozunguka Mji wa Itigi ili kuepusha mafuriko.

**WIZARA YA UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:**

**115. MHESHIMIWA SALIM MUSSA OMAR (GANDO):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo:-

Je, kwa nini baadhi ya mechi za Ligi Kuu ya Tanzania zisichezwe kwenye Viwanja vya Gombani na Amani vilivyopo Pemba na Unguja.

**WIZARA YA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:**

**116. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (BLW):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki:-

Je, Diplomasia ya Uchumi ina mchango gani katika kuleta mapinduzi kwenye Sekta ya Sayansi,Teknolojia na Uzalishaji.

**WIZARA YA FEDHA:**

**117. MHESHIMIWA ASIA ABDUKARIM HALAMGA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Fedha:-

Je, Serikali inatoa kauli gani juu ya GPSA kuchelewesha ununuzi wa magari ya Serikali.

**WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI:**

**118. MHESHIMIWA ANGELINA ADAM MALEMBEKA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi:-

Je, kuna mpango gani wa kudhibiti Kampuni Binafsi za Ulinzi ili kuhakikisha haziendi kinyume na maadili ya kazi zao.

## WIZARA YA MAJI:

**119. MHESHIMIWA STELLA SIMON FIYAO (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji:-

Je, kuna mpango gani wa kupeleka maji safi na salama katika Shule za Msingi na Sekondari nchini.

**120. MHESHIMIWA NOAH LEMBURIS SAPUTU (ARUMERU MAGHARIBI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji:-

Je, lini maji yatasambazwa Kata ya Mlangarine, Vitongoji vya Longipa, Mbuni, Olkereyan, Olmaroroi na Shule ya Msingi Muungano.

## WIZARA YA NISHATI:

**121. MHESHIMIWA MARGARET SIMWANZA SITTA (URAMBO):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nishati:-

Je, lini Serikali itakamilisha ujenzi wa kituo cha kupoza umeme Wilayani Urambo ili kumaliza tatizo la kukatika kwa umeme.

**122. MHESHIMIWA ISSA ALLY MCHUNGAHELA (LULINDI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nishati:-

Je, ni kwa nini Vitongoji vinavyopitiwa na mradi wa kuweka umeme migodini vinaachwa bila umeme - Lulindi.

**WIZARA YA MALIASILI NA UTALII:**

**123. MHESHIMIWA HASSAN ZIDADU KUNGU (TUNDURU KASKAZINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii:-

Je, lini Serikali itaweka mpango wa kukabiliana na wanyama wakali wanaosababisha vifo na hasara ya mazao kwa Wananchi wa Tunduru.

**WIZARA YA AFYA:**

**124. MHESHIMIWA FATMA HASSAN TOUFIQ (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:-

Je, Ni Watanzania wangapi wenye tatizo la *Sickle cell* na ni Mikoa mingapi imeathiriwa sana na ugonjwa huu.

**WIZARA YA MIFUGO NA UVUVI:**

**125. MHESHIMIWA FRANCIS KUMBA NDULANE (KILWA KASKAZINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mifugo na Uvuvi:-

Je, kuna mpango gani wa kuhamisha mifugo kutoka Wilaya ya Kilwa kwenda katika maeneo mengine nchini.

**III. KAMATI YA MIPANGO:**

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (MIPANGO NA UWEKEZAJI):**

Kwamba, Bunge lipokee, kujadili na kushauri kuhusu Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa unaokusudiwa kutekelezwa na Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025.

**WAZIRI WA FEDHA:**

Kwamba, Bunge lipokee, kujadili na kushauri kuhusu Mapendekezo ya Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025.

***(Majadiliano yanaendelea)***

**DODOMA** | **N.J. MWIHAMBI, *ndc***
**08 NOVEMBA, 2023** | **KATIBU WA BUNGE**